# TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA HALMASHAURI ZOTE NCHINI

**Ndugu Wananchi,**

Ofisi ya Rais – TAMISEMI imekuwa ikifuatilia ukusanyaji wa Mapato katika Halmashauri zake ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri zote nchini.

Baada ya kumaliza zoezi la usuluhishi wa kibenki ***(Bank Reconciliation)*** takwimu zinaonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya **shilingi 553,390,075,912/=** zimekusanywa kati ya **shilingi 687,306,661,000/=** sawa na **asilimia 81** ya lengo.

**Mchanganuo wa makusanyo umegawanyika katika maeneo yafuatayo:-**

**(a) MAKUSANYO YA MAJIJI KIASILIMIA:**

Katika upande wa Majiji, Jiji la Dodoma limekuwa la kwanza kati ya Majiji yote sita ikiwa imekusanya **shilingi 25,058,290,000/=** kati ya **shilingi 19,326,914,686/=** sawa na **asilimia 130** ya lengo lake wakati Jiji la Mbeya lilikuwa la mwisho kwa kukusanya kiasi cha **shilingi 7,836,169,412/=** kati ya **shilingi 11,010,640,000/=** sawa na **asilimia 71** *(Jedwali Na. 1).*

**(b) MAKUSANYO YA MANISPAA KIASILIMIA:**

(i) Kwa upande wa Manispaa; Manispaa ya Iringa ndiyo ilikuwa ya kwanza kwa kukusanya jumla ya **shilingi 4,283,112,132/=** kati ya **shilingi 4,172,846,000/=** sawa na **asilimia 103** ikifuatiwa na Manispaa ya Temeke iliyokusanya **shilingi 29,409,221,122/=** kati ya lengo la kukusanya **shilingi 29,066,936,000/=** sawa na **asilimia 101.** Manispaa ya Ilemela ilikuwa ya mwisho kwa kukusanya **shilingi 4,758,031,820/=** kati ya lengo la kukusanya **shilingi 11,753,610,000/=** sawa na **asilimia 40** *(Jedwali Na. 2).*

**(c) MAKUSANYO YA HALMASHAURI ZA MIJI KIASILIMIA:**

(i) Kwa upande wa Halmashauri za Miji, Halmashauri ya Mji wa Geita ndiyo ilikuwa ya kwanza kwa kukusanya jumla ya **shilingi 6,863,169,216/=** kati ya lengo la kukusanya **shilingi 3,150,910,000/=** sawa na asilimia 218 ikifuatiwa na Halmashauri ya Mji wa Njombe iliyokusanya **shilingi 2,927,610,757/=** kati ya lengo lake la kukusanya **shilingi 2,403,590,000/=** sawa na **asilimia 122** wakati Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ilikuwa ya mwisho kwa kukusanya **shilingi 1,135,016,934/=** kati ya lengo lake la kukusanya **shilingi 2,111,890,000/=** sawa na **asilimia 54** *(Jedwali Na. 3).*

**(d) MAKUSANYO YA HALMASHAURI ZA WILAYA KIASILIMIA:**

**(i)** Kwa upande wa Halmashauri za Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ilikuwa kinara kwa kukusanya jumla ya **shilingi 3,091,659,496/=** kati ya **shilingi 1,872,985,000/=** sawa na **asilimia 165** ikifuatiwa na Halmashauri ya Mpimbwe iliyokusanya **shilingi 1,552,516,085/=** kati ya **shilingi 956,837,000/=** sawa na **asilimai 162.**

(ii) Halmashauri za Wilaya zilizofanya vibaya zaidi ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iliyokusanya **asilimia 20,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliyokusanya **asilimia 33,** Halmashauri ya Rorya ilikusanya **asilimia 37** na Halmashauri ya Siha iliyokusanya **asilimia 39** *(Jedwali Na. 4).*

**(e) MLINGANISHO WA MAKUSANYO KIASILIMIA KWA MAKUNDI YOTE:**

(i) Katika mlinganisho wa kiasilimia kwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa bila ya kujali hadhi zao, Halmashauri tatu kinara kwa makusanyo kiasilimia ni Halmashauri ya Mji wa Geita ambayo imekusanya kwa **asilimia 218,** Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ambayo imekusanya kwa **asilimia 165** na Halmashauri ya Mpimbwe iliyokusanya kwa **asilimia 162** *(Jedwali Na. 5).*

(ii) Vivyo hivyo, Hamashauri tatu ambazo zimekusanya kwa asilimia ndogo zaidi ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iliyokusanya kwa **asilimia 20,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea **asilimia 33** na Halmashauri ya Wilaya ya Rorya iliyokusanya kwa **asilimia 37** *(Jedwali Na. 5).*

(iii) Katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya Halmashauri 38 sawa na asilimia 24 ya Halmashauri zote nchini ziliweza kuvuka malengo yake ya mwaka. Orodha ya Halmashauri hizo imeambatishwa *(Jedwali Na. 5).*

(iv) Vivyo hivyo, jumla ya Halmashauri 14 sawa na asilimia 7.57 hazikuweza kufikia asilimia 50 ya malengo yake. Halmashauri hizo ni kama inavyoonesha katika *Jedwali Na. 5.*

## (f) MLINGANISHO WA WINGI WA MAKUSANYO KWA MAKUNDI YOTE:

(i) Katika mlinganisho wa wingi wa makusanyo kwa Halmashauri zote bila kujalisha hadhi wala asilimia ya makusanyo, Mamlaka nne ziliibuka kinara kwa kukusanya mapato mengi. Manispaa ya Ilala ilikuwa kinara kwa kukusanya jumla ya **shilingi 44,505,151,623/=,** ikifuatiwa na Kinondoni iliyokusanya jumla ya **shilingi 29,754,382,565/=,**

Temeke ilikusanya jumla ya **shilingi 29,409,221,122/=** na Dodoma ilikusanya jumla ya **shilingi 25,058,290,451/=**.

(ii) Vivyo hivyo, Halmashauri tatu zilizokusanya mapato kidogo bila kujalisha asilimia ya makusanyo yao ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko iliyokusanya **shilingi 347,150,693/=,** Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe iliyokusanya **shilingi 371,224,164/=** na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iliyokusanya **shilingi 418,789,488/=** *(Jedwali Na. 6).*

**(g) MAKUSANYO KIMKOA:**

(i) Kwa upande wa Mikoa, Halmashauri za Mikoa mitatu ziliifanya Mikoa yao kuwa kinara kwa makusanyo ya mapato ya ndani. Mikoa hiyo iliongozwa na **Dodoma** iliyokusanya kwa **asilimia 170,** ikifuatiwa na **Geita** iliyokusanya kwa **asilimia 104** na Mkoa wa **Njombe** uliokusanya kwa **asilimia 103** *(Jedwali Na. 7).* Mikoa hii mitatu ndiyo iliyovuka malengo yake katika ukusanyaji wa mapato.

(ii) Mikoa mitatu ambayo ilikusanya kwa asilimia ndogo ni pamoja na Ruvuma uliokusanya kwa **asilimia 46,** Simiyu **asilimia 59** na Shinyanga **asilimia 66** *(Jedwali Na. 7).*

## MKAKATI WA KUIMARISHA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

a) Halmashauri zote zilizokusanya **chini ya asilimia 50** ya lengo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 nimezielekeza kutoa maelezo ni kwanini hazikufikia hata asilimia 50 ya lengo walilojiwekea.

b) Nawaelekeza Wakuu wa Mikoa kufuatilia ufujaji wa mapato katika Halmashauri zilizopo kwenye Mikoa yenu ili kubaini wanaohusika kufanya uzembe wa aina yoyote uliojitokeza katika ukusanyaji wa mapato kwenye Halmashauri hizo ili endapo itabainika kulikuwa na hujuma ya makusudi kwenye ukusanyaji chukueni hatua za kinidhamu na kisheria.

c) Mkakati wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kila Halmashauri katika Mikoa yote isikusanye chini ya **asilimia 81** ya lengo lake. Hivyo, Wakuu wa Mikoa mnapaswa kusimamia mkakati huu katika Mikoa yenu.

d) Wakuu wa Mikoa simamieni Halmashauri zenu ili kudhibiti matumizi ya mapato ya ndani yanayokusanywa kwa lengo la kufanikisha Miradi ya maendeleo kwa wananchi.

*Taarifa hii inapatikana katikia Website yetu: www.tamisemi.go.tz*

Nawashukuru sana.

Selemani S. Jafo (Mb.)

**05/10/2018** **WAZIRI WA NCHI (T)**